

HALMASHAURI YA MJI KASULU

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi wa Mji)



Simu: +255282810335

Tovuti: www.kasulutc.go.tz

Baruapepe: td@kasulutc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji

Halmashauri ya Mji Kasulu

S. L. P 475

KASULU.

KUMB NA. KSTC/D1/5

22 AGOSTI, 2024

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Mji Kasulu amepokea kibali cha ajira mpya kwa Ikama ya mwaka 2023/2024 kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishiwa Umma na Utawala Bora chenye Kumbu Na. FA.228/613/01/C/021 cha tarehe 25 Juni, 2024. Hivyo watanzania wote wenye sifa wanatangaziwa kutuma maombi ya kazi kwa nafasi zifuatazo;

1.1 MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II (INARUDIWA) - NAFASI 1

1.1.1 MAJUKUMU YA KAZI.

- i. Kuorodhesha kwenye rejestra barua zote zinazoingia Masjala (*Incoming Correspondence Register*)
- ii. Kuorodhesha kwenye rejestra barua zinazotoka nje ya Halmashauri (*Outgoing Correspondence Register*).
- iii. Kusambaza majalada kwa watendaji (*Action Officers*).
- iv. Kupokea majalada yanayorudi masjala kutoka kwa watendaji (*Action Officers*)
- v. Kutafuta kumbukumbu au nyaraka au majalada yanayohitajika na watendaji.
- vi. Kurudisha majalada kwenye Shubaka Kabati la Majalada (*Racks/Filling Cabinets*) au mahala pengine yanapohifadhiwa.
- vii. Kufuatilia mzunguko wa majalada ndani na nje ya Taasisi (*File tracking*)

1.1.2 SIFA ZA MWOMBAJI.

Mwombaji awe na Elimu ya Kidato cha Nne (Form IV) au Kidato cha Sita (Form VI) aliye hitimu na kupata cheti cha Mtihani wa Kidato cha Nne (Form IV) au Kidato cha Sita (Form VI) na kuhitimu mafunzo ya Stashahada (Diploma) (NTA LEVEL 6) katika Fani ya Utunzaji wa kumbukumbu kutoka vyuo vinavyotambuliwa na Serikali.

1.1.3 NGAZI YA MSHAHARA.

Kwa kuzingatia ngazi ya Mishahara ya Serikalini, **TGS C.**

MASHARTI YA JUMLA

- i. Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania wenye umri wa Kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45
- ii. **Waombaji wenye ulemavu wanahamasishwa kutuma maombi na wanapaswa kuainisha kwenye mfumo wa kuombea ajira aina ya ulemavu walionao kwa ajili ya taarifa kwa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishiwa Umma**
- iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi ya nayo jitoshaleza (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) wa kuaminika.
- iv. Waombaji ambao tayari ni watumishi wa Umma wapitishe barua zao za maombi ya nafasi ya kazi kwa waajiri wao.
- v. Maombi yote yaambatane na nakala ya vyeti vya Elimu na taaluma vilivyothibitishwa na Mwanasheria / Wakili ambavyo ni vyeti vya kidato cha Nne/Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika. **Diploma/Certificate, Cheti cha mtihani wa Kidato cha IV na VI, Computer Certificate, Vyeti vya Kitaaluma.**
- vi. Testimonials, “Provision Results”, “Statements of Results”, hati ya matokeo ya kidato cha Nne na Sita **HAVITAKUBALIWA**
- vii. Waombaji wa liosoma nje ya nchi wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na vimethibitishwa na mamlaka husika (**TCU, NECTA na NACTE**).
- viii. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wanakibali kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi.

ix. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria

x. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **28 OKTOBA, 2024**

xi. **MUHIMU:**Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu, anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa:-

Mkurugenzi wa Mji,
Halmashauri ya Mji Kasulu,
S.L.P 475,
KASULU.

xii. Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia anwani ifuatayo; <https://portal.ajira.go.tz/> (Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu ilioandikwa ‘*RecruitmentPortal*’).

xiii. Maombi ya takayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili **HAYATAFIKIRIWA.**

Limetolewa na,

MKURUGENZI WA MJI
HALMASHAURI YA MJI
KASULU